# KISWAHILI LUGHA

# DARASA LA NANE

# FOR K.C.P.E 2015

**AVAILABLE ONLINE AT:**

Schools Net Kenya Consultancy

**P.O. Box 8076 – 00200 Nairobi, Kenya | Tel: +254202319748**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com | www.schoolsnetkenya.com**

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **11.** Chagua kitenzi kilichonyambuliwa vizuri.

    A. Kimbia - kimbisha
    B. Waka - wakisha
    C. Ogopa - ogofya
    D. Oa - olesha

    Jibu sahihi ni C

    **1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [▬] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaalo zaidi.*

Mustakabali wa taifa hili ____ **1** ____ vijana. Ili uchumi ____ **2** ____ kuimarika, vijana wa ____ **3** ____ zote; *yaani* wa kiume kwa wa kike washirikishwe ____ **4** ____. Elimu wapewayo ____ **5** ____ isiwe tu ile ya kujipatia shahada mbalimbali na kushindwa kuyatumia maarifa haya ____ **6** ____ majukumu mbalimbali. Chambilecho wahenga, ____ **7** ____. Itakuwa busara kubwa ____ **8** ____ vijana hawa watasomea taaluma ambazo zitawawezesha kujiajiri, mathalani ____ **9** ____.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. unategemewa na | B. unahitajika | C. unawategemea | D. unafaa |
| **2.** | A. wetu uweze | B. yetu iweze | C. zetu ziweze | D. yetu uweze |
| **3.** | A. kabila | B. jinsia | C. namna | D. hirimu |
| **4.** | A. kamili | B. kiukamilifu | C. kikamili | D. kikamilifu |
| **5.** | A. nayo | B. nao | C. nako | D. navyo |
| **6.** | A. kutenda | B. kutekelezewa | C. kutekeleza | D. kutelekeza |
| **7.** | A. Elimu ni mali ambayo adui hawezi kuteka | B. Elimu bila amali ni kama nta bila asali | C. Akili nyingi huondoa maarifa | D. Maisha bila adha huwa malegevu |
| **8.** | A. laiti | B. angalau | C. ingawa | D. endapo |
| **9.** | A. useremala, utarishi na uashi | B. unahodha, upishi na uvuvi | C. uhandisi, uhunzi na usonara | D. ualimu, uhazigi na uhazili |

Michezo ya wanafunzi wa shule ____ **10** ____ manufaa ____ **11** ____ kwao. Hii ni kwa sababu ____ **12** ____ kuimarisha viungo vya miili ____ **13** ____, halikadhalika huujenga ____ **14** ____ miongoni mwao. Kila shule ____ **15** ____ kutenga sehemu na wakati maalum wa kushiriki michezo.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. wana | B. zina | C. yana | D. ina |
| **11.** | A. mengi | B. nyingi | C. mingi | D. mengine |
| **12.** | A. pia | B. mbali na | C. bali tu | D. kuliko |
| **13.** | A. wao | B. zao | C. yao | D. vyao |
| **14.** | A. ushirikina | B. ukiritimba | C. utegemezi | D. utengamano |
| **15.** | A. haina budi | B. ina budi | C. hawana budi | D. hazina budi |

*Kuanzia swali la **16** mpaka **30**, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Chagua orodha yenye nomino za jumla pekee.
A. moshi, mchanga, moto
B. udaku, upole, hofu
C. gari, mtoto, saa
D. halaiki, genge, kikosi

**17.** Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi:
Mwalimu alitaka kujua iwapo tungeondoka na wazazi wetu.
A. "Mngeondoka na wazazi wenu?" Mwalimu aliwauliza.
B. "Mtaondoka na wazazi wenu?" Mwalimu alituuliza.
C. "Mnaondoka na wazazi wenu?" Mwalimu alituuliza.
D. "Mngeondoka na wazazi wenu?" Mwalimu alituuliza.

**18.** Tumia nahau ifaayo zaidi kukamilisha sentensi hii:
Asha alilazwa hospitalini kutokana na ajali lakina sasa
A. amepata shufaa
B. amepata uradhi
C. amepata nemsi
D. amepata salama

**19.** Sentensi gani kati ya hizi ina kivumishi cha idadi?
A. Wengi waliofika waliujua ukweli
B. Wageni wetu walifika kwa wingi
C. Watu wote waliofika waliulizana maswali
D. Wazee kadhaa walifika hapo mkutanoni

**20.** Mavazi yapi ni ya watoto pekee?
A. Kizibau, kaniki
B. Kidotia, winda
C. Bombo, surupwenye
D. Kanzu, kashida

**21.** Ni ya kitenzi kishirikishi imetumika katika sentensi gani?
A. Wanafunzi wote wameenda michezoni
B. Mpunga mwingi ulipandwa kondeni
C. Mjombawe ni malenga stadi
D. Nitakupeleka kwake keshokutwa.

**22.** Andika methali nyingine yenye maana sawa na hii:
Angeenda juu kipungu hafikilii mbinguni.
A. Hakuna marefu yasiyo na mwisho.
B. Athari ya kidole hasara ya mwili.
C. Mpiga mbizi nchi kavu huuchunua usowe.
D. Pavumapo palilie si kazi kudamirika.

**23.** Katika sentensi zifuatazo, ipi haina masharti?
A. Usipokuwa na msu adui mbusu.
B. Ungejua alacho nyuki asali usingeiramba.
C. Nilipomwona alikuwa akimenya muhogo.
D. Ningalikuona ningalikujuza yote.

**24.** __________ ni kikembe cha bata.
A. Kivinimbi B. Kiyoyo
C. Kinyemere D. Kilebu

**25.** Jaa ni upande wa kaskazini. Maana nyingine ni
A. eneo la utawala
B. tamani chakula
C. kisawe cha ukubwa
D. fikia pomoni

**26.** Kihusishi cha mahali kinapatikana kwenye sentensi ipi?
A. Paka wangu ameketi juu ya meza.
B. Usinywe dawa kabla ya saa sita.
C. Uga wa mpira umefyekwa tena.
D. Nitamtembelea kwa minajili ya kumpa pole.

**27.** Tegua kitendawili kifuatacho:
Baba kalala ndani lakini ndevu zipo nje.
A. nyuni kiotani
B. hindi bichi
C. beberu zizini
D. mchwa kichuguuni

**28.** Sentensi ipi iliyo katika kauli ya kutendea?
A. Mtoto ameletewa zawadi
B. Sasa tutatembea haraka
C. Uzi huo umelegea sana.
D. Rehema anasomea kwa mjombawe.

**29.** Kisawe cha neno soko ni
A. mnada B. mshitiri
C. gulio D. konde

**30.** Kutokana na kitenzi ogopa, tunapata nomino
A. ogofya B. ogopesha
C. mwongofu D. wogo

*Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali* **31 – 40**

Uimara wa Kiswahili katika siku za hivi karibuni ni jambo la kutia mbwembwe. Japo hivyo, kuna haja ya kuongeza uwezo wa Kiswahili wa kutumika katika nyanja zote muhimu za maisha ya kisasa. Serikali imechukua dhamana na kuiinamia ndaro hii.

Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii tukufu, rasimu ya katiba mpya imekitaja Kiswahili kama lugha rasmi. Lugha hii sasa ina hadhi sawa na Kiingereza. Kwa mujibu wa sheria, Kiswahili ambacho pia ni lugha ya taifa, itatumiwa katika shughuli rasmi sambamba na Kiingereza. Shughuli hizi ni pamoja na makongamano, biashara, mawasiliano na kumbukumbu za kiutawala na shughuli za mahakama kuu. Inatia ari kuona kuwa itawezekana mikataba ya kimataifa kuandikwa kwa Kiswahili. Tayari katiba yenyewe imeandikwa kwa Kiswahili.

Ili kuyapa mambo haya msukumo, serikali imeafiki kuundwa kwa vyombo fulani muhimu. Moja ya hivi ni taasisi ya Kiswahili ya Kenya. Azma ya taasisi hii ni kuinua hadhi ya Kiswahili hata zaidi kwa kuifanya utafiti na kuimarisha ufundishaji wake katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Aidha taasisi ina haja ya kuhimiza uchapishaji wa maandishi mengi kuhusu lugha hii. Kizuizi cha kutekeleza haya ni upungufu wa istilahi zifaazo. Taasisi ya Kiswahili inajikakamua kutafuta, kuunda na kusambaza istilahi. Katika nyanja za sayansi, uhandisi, utabibu na teknolojia ya habari na mawasiliano.

Halikadhalika kumeundwa baraza la lugha katika wizara ya utamaduni, vijana na jinsia. Kutokea sasa na kuendelea, itawezekana masuala kuhusu Kiswahili kushughulikiwa katika ngazi ya kitaifa. Baadhi ya mambo yanayopasa kulishughulisha baraza hili ni matumizi mabaya ya Kiswahili. Hali hii hubainika katika vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na magazeti. Matumizi ya Kiswahili yasiyo sanifu pia hujitokeza katika mikutano ya kuitawala na kisiasa pamoja na sherehe na hafla mbalimbali.

Serikali inapojitahidi kuikuza na kuisambaza lugha ya Kiswahili tujihadhari na mtindo wa lugha hii kukopa kikasuku ustaarabu wa nchi za kimagharibi. Tayari jambo hili linapenyeza kucha zake kupitia tovuti, video, filamu na maandishi. Mavazi, vyakula na muziki wa kufokafoka ni tishio kubwa kwa lugha yetu jamala. Serikali haina budi <u>kulitilia guu</u> na kudhibiti mambo. La sivyo, kuna hatari, tena kubwa sana ya mienendo ya kigeni kuuangamiza utamaduni wetu ambao tumekuwa tukijaribu kuujenga upya tangu tulipopata uhuru.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
- A. kuimarika kwa Kiswahili kumefikia upeo sasa.
- B. Kiswahili kina nafasi nzuri ya kuimarika.
- C. Kiswahili ni lugha imara tangu zamani.
- D. Kuimarisha Kiswahili ni jukumu la kuachiwa serikali.

**32.** Mwandishi anasema wazi kuwa
- A. katiba mpya imekifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi.
- B. historia yetu haikukitambua Kiswahili.
- C. katiba ya nchi yetu imepuuza umuhimu wa Kiswahili.
- D. kielelezo cha katiba kimependekeza Kiswahili kuwa lugha rasmi.

**33.** Hivi sasa, Kiswahili kitatumika
- A. pamoja na Kiingereza katika shughuli rasmi.
- B. badala ya Kiingereza katika shughuli za kitaifa.
- C. kama lugha nyinginezo katika makongamano na mahakama.
- D. zaidi ya Kiingereza katika ujenzi wa taifa.

**34.** Katiba imeandikwa kwa Kiswahili
- A. ili iweze kusomeka kwa urahisi
- B. ili iweze kueleweka na wote
- C. maadamu kinapendwa kuliko Kiingereza.
- D. ili iweze kueleweka na wengi

**35.** Lipi <u>si</u> jukumu la Taasisi ya Kiswahili ya Kenya?
- A. Kuinua hadhi ya Kiswahili nchini.
- B. Kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili shuleni na vyuoni.
- C. Kuchapisha maandishi mengi ya Kiswahili.
- D. Kusambaza istilahi katika nyanja mbalimbali.

**36.** Baraza la lugha nalo lina jukumu lipi?
- A. Kushughulikia masuala mbalimbali ya Kiswahili kitaifa.
- B. Kusimamia wizara ya utamaduni, vijana na jinsia.
- C. Kubuni vifungu vya kuimarisha Kiswahili kikatiba.
- D. Kutunga na kuhakiki mitihani ya Kiswahili nchini.

**37.** Matumizi mabaya ya Kiswahili katika vyombo vya habari na mawasiliano yana madhara <u>makuu ya</u>
- A. kupotosha hadhira pana zaidi.
- B. kuwapotosha wanafunzi wa shule.
- C. kupotosha maana ya ujumbe uliolengwa.
- D. kukopa maneno ya lugha za kigeni.

**38.** Neno lipi la Kiswahili limekopwa katika orodha hii?
- A. Kurunzi
- B. Utamaduni
- C. Kiazikikuu
- D. Shati

**39.** Kuiga kikasuku hakufai kwa kuwa
- A. tunayo lugha yetu tukufu.
- B. uigaji haufai asilani.
- C. yote yaigwayo ni ya kupotosha.
- D. hufifilisha utamaduni wetu.

**40.** Maana ya <u>kulitilia guu</u> kulingana na muktadha ni
- A. kuzuilia mafanikio
- B. kuingilia kati
- C. kulipigia debe
- D. kula kiapo

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41 – 50***

Tamasha alikuwa kabandikwa jina la kebehi "Vuna ulichopanda". Hakuna yeyote pale kijijini aliyeweza kukitegua kitendawili cha jina lake hili jipya. Ungemwuliza ungemsikia akisema, "Babu we! Dunia ina mambo."

Siku moja nilikutana na Tamasha njiani akielekea kondeni ambako alipitisha mchana wote siku nenda siku rudi. Baada ya kujuliana hali naye nilijiambia kuwa nijaribu bahati yangu. Nikapiga moyo konde na kumwuliza kwa nini yeye hupenda kuyahudumia makonde yake kila siku. Tamasha aliniangalia kwa jicho pekuzi lililopenya hadi kwenye mtima wangu. Akaangua cheko la simanzi na kuniambia, "kijana utakapokua utajua kwamba ukupigao ndio ukufunzao."

Tamasha kama alivyokuja kunieleza baadaye, alikuwa mwana aliyezalika na kulelewa vyema. Baada ya kukamilisha masomo yake ya chuo kikuu, aliajiriwa na kampuni mojawapo ya kuuza mafuta. Alikuwa mcha Mungu hadi siku moja, baada ya kuajiriwa kazi mjini alipopata ufa kwenye tabia yake. Mshahara aliopata ulidinda kabisa kuyakimu mahitaji yake mengi. Akawa kila mara hata kabla ya tarehe kumi na tano, yu waya. Baada ya kujikuna kichwa kwa muda, alipata suluhisho la hali yake ya uhitaji akaunyoosha mkono wake kuiambia kalamu yake itwae mali ya kampuni.

Miaka ya mwanzomwanzo mambo yalimwendea salama. Akatononoka, kipaji kikamnawiri. Hata hivyo serikali katika shughuli za kupigana na ufisadi iliurefusha mkono wake zaidi. Watu wa hulka na kimo cha Tamasha wakawa mashakani. Siku moja, baada ya Tamasha kufanikiwa si haba katika mradi mmoja wa "maendeleo" ,alikutana na mkwewe. Alitiwa mbaroni na hatimaye kuhukumiwa kifungo cha miaka saba.

Tamasha alitoka gerezani baada ya miaka minne unusu. Alibahatika kuwa miongoni mwa waliofunguliwa na rais siku ya Jamhuri. Tangu siku hiyo Tamasha ameuvaa moyo mpya. Amepania kula jasho lake mwenyewe. Aliyanunua makonde yake mawili na kuanzisha shughuli za ukulima. Maisha ya anasa mjini aliyapa kisogo. Tamasha kila mara hakusita kuwahimiza watu kutokuwa wakunguni na vimelea. Ingawa hakuweza kumpata mke kwa sababu ya fikira za walimwengu kuwa, "Mwenye kavu sidhani kapoa", yeye alitosheka na kidogo alicho nacho. Haachi kuwakumbusha adinasi hususan vijana maana ya methali "Bura yangu sibadili na rehani."

41. Jina la kebehi alilobandikwa Tamasha lilikuwa la
A. kumtania
B. kuficha asili yake
C. kumwudhi
D. jina lake halisi

42. Mwandishi anaposema alitaka 'kujaribu bahati yake' lengo lake lilikuwa
A. kujua kiini cha Tamasha kuenda shambani.
B. kuelewa kwa nini Tamasha alichukiwa na watu.
C. kujua alikoshinda Tamasha kila siku.
D. kufichuliwa siri ya maisha ya Tamasha.

43. Maana ya nikapiga moyo konde ni
A. nikavumilia
B. nikajikaza
C. nikajilazimisha
D. nikajiimarisha

44. Kulingana na kauli ya Tamasha kwa mwandishi
A. mtu huyafurahia mabaya anapoyatenda ila hujuta baadaye.
B. watu wote fisadi hufungwa gerezani.
C. adhabu humfunza mtu mwenendo na tabia ifaayo.
D. huwezi kueleza madhara ya jambo usilolifahamu.

45. Chagua kauli sahihi kulingana na makala:
A. Maisha ya Tamasha ya utotoni hayakuwa na dosari.
B. Tamasha alianzisha kampuni ya kuuza mafuta.
C. Tamasha mwenyewe hakupenda kuoa.
D. Tamasha hakuweza kujipatia shahada.

46. "Alipopata ufa kwenye tabia yake", ndiko kusema
A. maisha yake yaliporomoka.
B. mienendo yake iliingia doa.
C. tabia zake ziliharibika kabisa
D. hapo ndipo alipoachishwa kazi

47. Kwa nini mshahara wa Tamasha haukumtosha?
A. Mshahara ulikuwa mdogo
B. Alikuwa na wategemezi wengi
C. Alifanya kazi ya kijungujiko
D. Alikuwa mpenda anasa

48. Njama za Tamasha zilifikia hatima kwa kuwa
A. serikali ilijizatiti kupambana na ufisadi.
B. hakuweza kuficha hila zake sawasawa.
C. wenzake kazini waliamua kumshtaki.
D. maendeleo yake ya ghafla yalitiliwa shaka.

49. Maoni ya mwandishi wa makala ni kuwa
A. msamaha wa rais hubadili mienendo ya wengi.
B. starehe hufanya watu waingilie ufisadi.
C. jamii haisadiki kuwa waovu wanaweza kubadilika.
D. wengi watokao jela huingilia ukulima.

50. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni:
A. Cha kuzama hakina rubani
B. Siku za mwizi ni arubaini
C. Mui huwa mwema
D. Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo